NOVEMBA 2022

Lipakue sasa kupitia www.getvalue.co

# TULIZO

Kwa Habari Fasaha za Fasihi

CHAPA YA KUMI NA MOJA



3 KALI ZA NOVEMBA

## HUSSEIN TUWA

MZAZI, MUME, RAIS NA MWANDISHI TANGU 2002

## MIAKA 10 YA JAMVI LA SIMULIZI


MUASISI RICHARD MWAMBE ASEMA NASI

## MONEY BANK

WAZO LA MWANDISHI RAJAB SAID

BURE

jaridatulizo@gmail.com


Huyu Hapa
Bingwa Wa Taharuki
HUSSEIN ISSA TUWA
"Lengo langu lilikuwa kuiridhisha nafsi yangu kwa kufanya nikipendacho, na kuwaridhisha wasomaji kwa kazi zangu. Nilishavipata vyote hivyo, sasa nashindania nini?"

# ZIARA HAMSINI NA MOJA ZA BINGWA

Zamani nilizoea kusikia watu wakisema, "fulani kapigwa mvua saba" kwa kosa fulani. Wengine wakisema, "kala masika saba"... na vitu kama hivyo, wakimaanisha kuwa kafungwa jela "miaka" saba. Ina maana waliiwekea miaka tafsida ya kuifananisha na misimu ya mvua/masika.

Tarehe 6 Novemba mwaka huu nikijaaliwa uhai, nitatimiza miaka hamsini na moja ya kuzaliwa.

Tofauti na ilivyozoeleka, mimi naitazama miaka hii hamsini na moja kama ziara zangu hapa duniani mpaka sasa. Hivyo ndivyo (ziara) hamsini na moja za Tuwa zinapoingia kwenye picha. Kila mwaka wangu mmoja nautazama kama ziara moja hapa duniani. Na hakika, hakuna ziara mbili zinazofanana.

Kimsingi sote hapa duniani tumekuja kuzuru tu, kisha tunarudi tulikotoka, kwa Muumba. Hata hivyo, sio lengo langu kutoa mawaidha hapa. Ni kwamba, hapa nimesimama kwenye kizingiti cha kuiingia miaka hamsini na moja, halafu nageuka nyuma kuzitazama ziara zangu zilizopita, hususan mapito yangu katika uandishi wa riwaya.

Japo ziara zangu za uandishi zilianza tangu nikiwa na miaka 7 nilipoanza kujua kusoma na kuandika, ningependa zaidi kuzitazama (kuitazama) zile ziara (ile miaka) zinazoanzia mwaka 2002, ambapo kazi yangu ya kwanza, "MTUHUMIWA", ilitoka kwa mara ya kwanza kwenye gazeti la Kiu Ya Jibu.

Mapokeo yake yalinijaza ujasiri wa kuendelea kuandika. Na hapa nikapata somo kubwa sana lililojenga msingi wa maamuzi yangu ya baadaye, kuhusu uchapishaji wa vitabu. Lilikuwa ni somo chungu sana kwa kweli. Ila sitalijadili hapa.

Mwaka 2003 nikaandika "MKIMBIZI", (kitabu 2007). Jamii ikaniambia kuwa imenikubali rasmi kwenye tasnia.

Mwaka 2004, nikaandika "MFADHILI", na Mwaka 2005 ikanipatia tuzo yangu ya kwanza kwenye fasihi - McMillan Aidan Award for African Literature! Kitabu kikaingia kwenye mtaala wa elimu nchini.

Kwa kweli hapa hata mimi mwenyewe nilianza kuogopa. Nikajitafakari sana jinsi safari yangu ya uandishi ilivyoanza kwa mafanikio namna vile. Nilijua kuwa, kadiri unavyozidi kupaa, ndivyo mweleka unavyokuwa mkubwa zaidi. Nikajiuliza. Je, ni kwamba naandaliwa kwa mporomoko mkali zaidi?

Nikatulia kidogo.

Mwaka 2013 riwaya yangu ya kizungu "TEMPORARY ORPHAN", ikanipatia Tuzo yangu ya pili, The Burt Award Literature for Young Adults. Ikaniweka kwenye daraja jingine.

Katika ziara zangu hizi, nimeweza kuandika pia riwaya za: MDUNGUAJI (2006), UTATA WA 9/12 (2012), MTUHUMIWA (kitabu–2015) BONDIA (2016), WIMBO WA GAIDI (2017), MTAFITI (2019). Na 2021 "MISS TZ."



Si haba kwa kweli.

Si hivyo tu, ziara zangu zimenipitisha kwenye mengi mengine ndani ya uandishi. Naangalia jinsi nilivyotegwa na wasomaji kwa kushindanishwa na waandishi wakubwa wa wakati huo. Na jinsi nilivyoukwepa mtego huo mbaya.

Nilijua kuwa lengo langu la kuanza kuandika halikuwa kushindana na yeyote kati ya walionitangulia au nilioingia nao kwenye fani.

Nilijua, kwenye mashindano kuna matokeo mawili - kushinda au kushindwa. Lakini zaidi, nilijua kuwa usiposhindana, hushindwi.

Lengo langu lilikuwa kuiridhisha nafsi yangu kwa kufanya nikipendacho, na kuwaridhisha wasomaji kwa kazi zangu. Nilishavipata vyote hivyo, sasa nashindania nini?

Nikaamua kushindanisha kazi zangu zenyewe kwa zenyewe, ili nisijibweteke.

Na matokeao yake hayajawa mabaya, Al Hamndu Lillaah!

Nautazama uzinduzi wa kitabu changu cha MTAFITI pale Makumbusho ya Taifa, tarehe 23 Septemba 2019, ambapo kwa mara ya kwanza niliona watu wakipanga foleni kununua kitabu cha fasihi ya Kiswahili.

Natazama jinsi tulivyofanikiwa kuunda umoja wetu wa UWARIDI, na mafanikio na changamoto nilizokutana nazo ndani ya umoja huu.

Nautazama MFUKO WA RIWAYA WA UWARIDI, na jinsi tulivyoweza kutoa vitabu vitano kwa nguvu zetu wenyewe mpaka sasa.

Nalitazama tukio kubwa kabisa kupata kutokea linalohusu vitabu, waandishi na wasomaji, tukio la MJUE MTUNZI.
Naitazama NGAO YA MTUNZI niliyoipata kupitia jukwaa hili la MJUE MTUNZI.

Hakika, kuna somo kubwa sana nimevuna kuhusu tasnia yetu kupitia UWARIDI.

Naweza nikaendelea weee, mpaka mkaboreka, kama bado hamjaboreka mpaka sasa.

Itoshe tu kusema kuwa, haya yote hapo nyuma, ndiyo yamekuwa msingi wa maamuzi yangu kwenye uandishi, kwa mtaji wa ziara zangu "hamsini na moja".

Ndiyo leo najikuta nasimama kwenye kizingiti cha miaka hamsini na moja ya ziara zangu hapa duniani.

Je, nimekuwa na athari ipaswayo kwenye jamii ya wasomaji, na waandishi?

Ninapaswa nifanye nini zaidi baada ya hapa - nistaafu kuandika?

Sijui kwa kweli, ila yote kwa yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuyatimiza haya niliyoyatimiza kwenye uandishi mpaka sasa.

Nawashukuru wazazi, na familia yangu kwa kuniunga mkono kwenye kazi zangu za uandishi.

Nawashukuru waandishi wenzangu kwa kuwa sehemu ya mafanikio yangu kwa kunishauri, kushirikiana nami na kuniunga mkono, na kwa kunipa nafasi ya kuwashauri na kuwaongoza kama Rais wa UWARIDI.

Nawashukuru wauzaji wa vitabu nchini pamoja na wamiliki wa maduka ya vitabu, kwa kuendelea kuuza kazi zangu kila ninapozitoa, na zaidi… nawashukuru wasomaji wote kwa kuendelea kusoma na kununua kazi zangu.

Naamini, sijatimiza makubwa sana, lakini haya niliyoweza kuyafanya kwenye hizi ziara zangu hamsini na moja ndiyo majaaliwa yangu.



# 10 MIAKA JAMVI la SIMULIZI



## RICHARD MWAMBE KAMANDA AMATA

**NA MWANDISHI WETU**

Kwa wapenzi wa riwaya Tanzania hasa zile za kijasusi, jina hili SI geni kwao kwani tangu mwaka 2013 limekuwa likiwaburudisha katika uga huo.

JAMVI la SIMULIZI ni jukwaa la riwaya lililoasisiwa na Mwandishi Richard Mwambe au wengi humtambua kama Kamanda Amata.

Katika Siku hizi chache zilizopita, kupitia ukuta wake wa *Facebook* amekuwa akitusimulia juu ya safari nzima ya Jamvi la Simulizi, milima na mabonde mpaka sasa linakaribia miaka Kumi.

"Kuandika ni kitu kimoja na kuunda jukwaa la Wasomaji ni kitu kingine," anasema Mwandishi Richard Mwambe. Aidha anasema kwamba Mwandishi licha ya kuandika lazima ajue pia jinsi ya kujenga mashabiki.

Miaka Kumi ya *Jamvi la Simulizi* anaielezea kama safari ngumu sana aliyowahi kuisafiri kikalamu. Na anawataja wote walioshirikiana naye kwa namna moja au nyingine kutengeneza fan base yake.

*Richard MWAMBE* anamtaja *Andrew Carlos* kuwa ni mtu wa kwanza kumshika mkono na kumwonesha nini soko la kigijitali linataka. Huyu ndiye aliyemtangaza na kumtambuliaha kwa wapenzi wa riwaya. Nao wakampoke Kwa mikono miwili akiwa na riwaya yake ya Msitu wa Solondo.

Amata anamtaja *Frank Masai, Gadison Baita* na *Mtoto wa Beka* kama waandishi wenza waliochangia sana kuinua *Jamvi la Simulizi* kati ya Miaka *2013-2015.*

Kuhusu mafanikio ya jukwaa hilo, Amata anasema, “mafanikio yapo. Kwa miaka yote tisa tumeadika riwaya karibu 40 nyingi zikiwa za kichunguzi. Tumetoa vitabu vinne; ***Tufaa Jekundu 2015, Cronoc 7 2016, Mpatanishi 2018 na Harufu ya Kifo 2020.*** Bado tuna riwaya nyingi ambazo hazijafanywa vitabu ila mpango upo.”

Amata aliendelea kusema, “ukiachana na hilo, tukaanzisha jarida tepe ambalo tunalitumia kama sehemu ya kuwatangaza waandishi kwa kuweka kazi zao, kueleza safari zao za kiuandishi lakini zaidi ni kuijuza jamii kile ambacho waandishi wao wanafanya. Hili jarida linaitwa Ngurumo ya Mwandishi.”

Ukiachana na jarida, kupitia jukwaa la Jamvi la Simulizi wameanzisha NGO inaitwa Kitabu Maisha ambayo inafanya kazi na shule za sekondari za serikali kote Tanzania.

Kwa sasa Jamvi la Simulizi linasimamiwa yeye mwenyewe kama Muasisi na Rey Stanley kama mratibu.

“Tunapoelekea azimisho la MIAKA KUMI ya uwepo wa *Jamvi la Simulizi,* tunafikiri kuwapa shukrani wapenzi wa riwaya ambao wao ndiyo chagizo kubwa sisi kufika hapa.” Amata alisema .

“Tutafanya nini Kwa ajili Yao? Hilo tumeliweka kwenye mabano. Lakini 2023 tutakuwa na Siku maalum ya kufanya jambo na Wasomaji wetu.” alimaliza.

Kauli mbiu yao inasema *"Sisi tunaandika, ninyi mnasoma."*

Tulizo tunawatakia wana Jamvi la Simulizi kila la kheri.

# WAZO LA MWANDISHI



**SAID RAJAB**

# MONEY BANK

Nakumbuka wazo la kuiandika riwaya ya MONEY BANK lilianza nikiwa safarini, ndani ya gari binafsi tukiwa watu watatu. Ilitokea tu katika mazungumzo yetu, mmoja miongoni mwa watu tuliokuwepo pale garini alikitaja kisa cha wizi wa fedha uliotokea katika benki moja ya serikali katika nchi jirani ya Kenya. Ukweli ni kwamba aliyetaja kisa hicho alikitaja kwa ufupi sana, lakini hakujua ni kiasi gani nilikipenda kisa kile. Nilichelea kuomba kisa kile kiendelezwe kutokana na umuhimu wa mada iliyoingia katikati wakati kisa kile cha uporaji kikiwa kinasimuliwa. Hivyo nilichukua sehemu ileile fupi ya kisa kile na kukihifadhi kwenye sehemu ya kuhifadhia kumbukumbu kwa muda mrefu (longterm memory).

Baada ya kuachana na watu hao niliokuwa nao ndani ya gari, kila mmoja alishika hamsini zake, lakini mimi kisa kile kilinisumbua sana akilini. Kuanzia hapo, nilijaribu mara kadhaa kukitia kisa kile kwenye maandishi lakini nilishindwa. Hiyo ilikuwa ni mwezi wa tatu mwaka huu. Nilijaribu tena na tena, lakini kila mara niliona hakuna chochote chenye maana ninachoandika.

Wakati huo zilikuwepo hadithi zingine kadhaa ambazo tayari nilikwishazianza na zingine zilikwishakamilika lakini sikuzipa go ahead kutokana na sababu mbalimbali. Niliporejea masomoni semister iliyofuatia nikajikuta nimetingwa na ratiba za chuoni, lakini wazo la kuiandika MONEY BANK likawa bado linanifokea akilini.

Baada ya ile Semister kupita, nilirejea tena Zanzibar mji ambao wazo la kuiandika MONEY BANK lilichimbukia. Na hapa nikiri kuwa mazingira ambayo wazo limechipukia huwa na athari kubwa ya mwendelezo wa wazo hilo. Wakati nimerejea Unguja nilianza mara moja kuandika kwa hamu na raghba zaidi kwa kuwa niliamini kikwazo kilichonizuia nisiandike kwa kipindi kirefu (masomo) kilikuwa kimeondoka. Wakati huo nilikuwa nimeshafanya mtihani wangu wa mwisho wa chuo.

Hapo basi nilianza miswada mipya na kuiendeleza mingine, ikiwemo hadithi iliyopendwa sana kwenye kundi sogozi la WhatsApp niliyoipa jina la DISKO LIMEINGIA MMASAI. Wakati DISKO ikiendelea kusomwa kwa hamasa zote ghafla tu nilijikuta nikiihisi tena hamu ya kuiandika MONEY BANK, lakini mambo bado yakawa yaleyale. Nilikuwa nafeli zaidi katika namna ya kuiendeleza hadithi. Suala la kuanza si kazi kwangu, kwani mimi huwa naamini katika automatiki. Yaani pale ninapoanzia huwa si mimi, bali ni maandishi yenyewe yanajiandika, hivyo sijipi ujiko wa kuyakosoa maandishi ambayo nimeamua kujiandika yenyewe. Kwangu si tatizo pia kuona najaza maneno mengi yasiyo, kwani naamini kuwa ninayo nafasi ya kukisoma kile nilichokiandika na kukipangua hata mara kumi, kisha nikapata mtiririko mzuri wenye mantiki. Hivyo mpaka hapo utaona kuwa tatizo kubwa lililokuwa likinikabili wakati wote wa mwanzo kuiandika MONEY BANK ilikuwa ni ukomo wa mawazo ya kile ninachokiandika, ni leile waandishi wanayoiita writer's block.

Baada ya kupita kipindi kidogo, nikiwa safarini naelekea shamba moja inayoitwa MATEMWE iliyopo kaskazini mwa Unguja, ndipo wazo la namna ya kuiendeleza MONEY BANK lilivyopatikana. Ukiisoma riwaya hii, utakutana na kipande hiki.

"MWAKA 2015, siku hiyo Mzee Chande akiwa njiani ndani ya gari lake. Alikuwa akielekea mkoa wa Kaskazini, huko ilipo shamba moja inayoitwa Matemwe. Akiwa kwenye gari yake, siku hiyo alikuwa na mawazo sana. Njia nzima alikuwa akiyaangalia mandhari aliyokuwa akiyapita pasina hata kuyazingatia.

Akili yake ilikuwa mbali mno.

Lakini kama sadfa tu, ikatokea akamakinika na kitu kimoja alichokiona kwenye nyumba zilizokuwa pembezoni mwa barabara. Hapa alikuwa maeneo ya Kbweni, Bububu.

Kama bahati tu, macho yake yalikumbana na maduka mengi yaliyokuwa na neno lenye maana nzito sana kwenye maisha yake.

Mzee Chande licha ya kuwa mfanyabiashara maarufu wa nafaka, ambaye alijitafutia soko la nafaka kwenye hoteli za kitalii huko maeneo ya shamba, pia alikuwa na kazi nyingine ya siri. Mzee huyu alikuwa ni mafya. Alikuwa muuaji wa kutumwa. Kama utamwita The Hitman utakuwa sahihi. Fauka ya umafya, pia alikuwa ni wakala wa magenge ya uporaji kutoka nje ya nchi. Kila genge la ujambazi miongoni mwa magenge hayo yalimpatia jina maalumu la utambulisho wake. Kwenye moja miongoni mwa magenge hayo magenge hayo alijulikana kama "WAKALA namba 47."

Akiwa njiani kuelekea Matemwe, mawazo yaliyokuwa yakimuumiza kichwa chake kwa wakati huo, ilikuwa ni kwa jinsi gani ataweza kuikamilisha kazi aliyopewa na waajiri wake. Kazi yenyewe haikuwa ya kitoto. Ilikuwa ni kuipora hazina kubwa ya vito vya dhahabu iliyokuwa imehifadhiwa kwenye benki moja huko maeneo ya Kiembe Samaki. Pamoja na ugumu wa kazi hiyo aliyopewa, Mzee Chande alikuwa hodari wa kupangilia mbinu zake. Aliamini kuwa muda wowote atakaoingia ulingoni kupambana na adui yake, muda huo alitakiwa kuwa kama maji. Ilivyo, maji siku zote hukwepa miinuko na kufuata mteremko, lengo likiwa ni kuvikwepa vikwazo na kuzishambulia sehemu dhaifu.

Kwa mtindo huo, aliamini katika mbinu ya kivita isemayo, "mtu ataweza kushinda vita, ikiwa tu ataijua hali ya adui yake." Hatua ya kwanza ikawa ni kuitambua hali ya mfumo mzima wa benki ile. Ubora na udhaifu wake. Baada ya kuyatambua hayo yote, ndipo alipoijua njia itakayomwezesha kufanikisha kazi ya mabosi wake."

Kwenye kipande hiki nilichokinyofoa kwenye riwaya hii, ipo safari ya kuelekea Matemwe iliyofanywa na Mzee Chande. Tukio hili ni halisi na kweli kabisa. Ni mimi mwenyewe mwandishi ndiye niliyekuwa safarini siku hiyo, kisha wazo la jinsi ya mwendelezo wa hadithi yangu utakavyokuwa likapatikana kwenye safari hiyohiyo. Umeona jinsi mawazo ya kuandika yanavyopatikana kimazabe? Na hii hutokea zaidi kwenye visa korofi kama kilivyo kisa hiki cha MONEY BANK.


Najua utadhani kuwa hapo tayari kila kitu kilishakamilika, ikabakia tu kuandika. Hasha!

Baada ya hatua hizi mbili katika kuisogeza hadithi hii kwenye asilimia karibu 60, ikawa kasheshe ni kuzimalizia hizo 40 zilizobaki. Hizi bwana zilipatikana kwa idea zinazotoka kwenye filamu tunazozitizama. Na filamu yenyewe hata sikuitazama mimi, nilisimuliwa tu na mdogo wangu, ambaye hata jina la filamu yeye mwenyewe hakuwa analikumbuka.

Kwa mantiki hiyo, sitokuwa na uwanda mpana wa kuutaja mchango wa filamu hiyo kwenye hadithi hii ya MONEY BANK , ila nikiri kwamba filamu hiyo imekuwa na mchango mkubwa sana katika kuipamba hadithi yetu ya MONEY BANK. Dokezo ni kwamba, namna ya kuwatoa walinzi wote ndani ya benki na kuhamia nje ili kuwazuia waporaji wale wasimwibie Mzee Chande, idea ile ilipatikana kwenye filamu hiyo niliyosimuliwa.

Ni hivyo, kama isemwavyo siku zote kuwa fasihi si ombwe, kwamba uandike kitu ambacho hakipo kwenye maisha ya ulimwengu huu. Ilivyo, mtu huzungumza au kuandika kile ambacho macho yake yalipata kuoana au masikio yalipata kusikia. Hivyo mchango wa movie hii na zinginezo, pamoja na utafiti mbalimbali nilioufanya kwa kutembelea baadhi ya maeneo, kuperuzi mtandaoni nikiwa natafuta taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajilibya kuileta MONEY BANK kwenye uhalisia, hayo yote ni mambo yaliyofanikisha kukamilika kwa riwaya yetu hii.

Kwa kuhitimisha ni kwamba, ndani ya miezi kama nane niliyoitumia kuandika riwaya hii, msimuliaji wa kile tukio lililotukia kule nchini Kenya hakuwa na taarifa kuwa mimi nilikuwa nikihangaika kuihamishia simulizi hii kwenye maandishi. Lakini katika mwezi huu wa nane tangu ile siku tuliyokuwa ndani ya gari, nilikaa tena na yule bwana na kumuonyesha hatua niliyofikia katika kuiandika simulizi ya MONEY BANK. Jamaa alishangaa sana, akaniuliza kwa lugha ya kizungu, "My God! You turned my story into a novel!?" nilimjibu, "Yes, come and read




few chapters of it..!"

Jamaa alisoma kurasa kadhaa hapohapo kwenye kompyuta yangu huku akipatwa na hisia za furaha zilizoambatana na mshangao kwa mpigo mmoja. Kisha aliniuliza kuhusiana na utafiti juu ya tukio halisi. Kuwa labda nilishawahi kulifuatilia tukio lenyewe mtandaoni. Nilimjibu hapana, na nikamweleza kuwa sikufanya hivyo kwa kuhofia maandishi yangu kutekwa na uhalisia wa tukio halisi.

Nilihitajia MONEY BANK iwe hadithi bunilizi yenye uhalisia uliotokana na utashi wangu mwenyewe, na sio ule wa tukio halisi. Isingekuwa vibaya kulivisha tukio hili uhalisia wake kamili uliotiwa nakshinakshi za kifasihi, lakini mimi sikutaka hivyo. Ni mapenzi binafsi ndiyo yaliyoniongoza kulikwepa hilo na kuumiza kichwa katika kutafuta uhalisia wangu mimi mwenyewe.


Naam, kwa namna hiyo, asilimia 60 na zile 40 zilizobakia za MONEY BANK na vikorombwezo vingine vilivyoongezeka kama vile normalized power of language (nguvu ya lugha isiyotambuliwa na wengi), hadaa za mchezo wa bao la kete (chase body) na za namna nyingine kibao, hadithi hii ikawa imekamilika hivyo kwa kuandikwa katika kipindi cha miezi isiyopingua tisa.

***Tulizo tulihitaji kujua ka nini aliamua kutumia jina la Kiingereza kwenye kazi ya Kiswahili, alisema haya.***

Mwanzoni jina la Kiswahili ndilo lililoanza kunijia akilini, ambalo likikuwa ni WAKALA. Lakini baadaye nililibadilisha baada ya kuuangalia mwelekeo wa hadithi yangu na na pia katika kutafuta jina lenye ushawishi na mvuto zaidi, ndipo nilipotumia jina la mission ambayo ilitekelezwa na wahalifu ndani ya hadithi, ndilo nikalifanya jina la kitabu. Lakini katika kukinda utambulisho wa lugha ya Kiswahili, ndipo nilipoibuka na maneno Siri Mtegoni, Hazina Mkononi, angalau iwe ni ishara ya lugha iliyotumika ndani ya stori. Yote kwa yote ni sanaa tu ndiyo iliyopelekea hadithi hii kupewa jina la Kiingereza badala ya Kiswahili.

Ukawa mwisho wa mahojiano yetu kwenye wazo la mtunzi ambapo Rajab Said ameeleza vema mapito yake mazito wakati anaandaa kitabu cha Money Bank.

Tulizo Media tunamtakia kila la kheri kijana huyu kwenye uwanda huu wa fasihi andishi.




TULIZO MEDIA

***TULIZO MEDIA***

***Ni Muunganiko wa Kazi Sita.***

***1. Tulizo Graphics. Kazi yake ni kufanya kazi zote za ubunifu kama vile kufanya majalada ya hadithi, riwaya, tamthiliya, nyimbo, ushairi, kupanga kitabu, kuandaa mipango ya biashara nk.***

***2. Tulizo Studio, hii ni kwa ajili ya kuandaa kazi za sauti.***

***3. Tulizo Magazine. Hili ni jarida linaloruka kila mwezi.***

***4.Tulizo Printing. Kazi yake ni kuchapa kazi mbalimbali.***

***5. Tulizoflix. Huu ni ulimwengu wa filamu ambapo tulizo huzichambua.***

***6Tulizo Visual. Hapa ni kwenye kutengeneza videos na kupiga picha mbalimbali zenye viwango.***

***Kwa huduma wasiliana nasi kwa +255 627 585 638***



# Safari Ya Mtunzi

# Hussein Wamaywa

## Alipotoka na Anapoelekea

Nina umri wa miaka 42 sasa, ni mtu mzima sasa, uongo?. Historia yangu ya uandishi ilianza mwaka 1991 wakati huo nikiwa darasa la kwanza pale Shule ya Msingi Kiezya Kigoma. Mzazi wangu alichelewa sana kunipeleka shule ya msingi (Mie sikuanza shule ya awali) kwa hiyo vijana wa rika langu walipokuwa wakitoka shule walikuwa wakininyanyasa sana kwa kuwa nilikuwa sijui kusoma. Nilipoingia darasa la kwanza mwaka uliofuata, nilikuwa na hamu ya kujua kusoma kuliko kitu kingine chochote, na nilipomaliza zile herufi 26 yaani "A" hadi "Z", tayari nilikuwa najua kusoma. Na hapo nikaanza kusoma kila kitu. Kwa kuwa uelewa wangu haukuwa mkubwa, kitu pekee nilichokuwa nikikielewa ni hadithi. Namshukuru sana baba yangu Mzee Msafiri Wamaywa ambaye alikuwa na utamaduni wa kununua magazeti kila siku. Hapo ndipo nilipoanza kuzipenda hadithi na hazikupita siku nyingi nikakutana na mwenzangu mmoja aitwae Halfan ambaye alipenda hadithi pia. Tukajiunga Maktaba ya Mkoa wa Kigoma ambapo tulimaliza vitabu vyote vya hadithi vilivyokuwa Maktaba ndani ya siku 90 tu! Baada ya hapo tukawa hatuna cha kusoma. Ndipo tulipoanza kuandikiana hadithi. Mimi namundikia yeye asome na yeye ananiandikia mimi nisome. Hali hii iliendelea mpaka pale walipopata mgeni kwao ambaye hakuamini kama zile hadithi tuliandika sisi kutoka vichwani mwetu. Ubishi wake ulitufanya tuone kwamba tunaweza na safari ya utunzi ikaanzia hapo rasmi.

Nje ya hapo historia yangu kwa ufupi ni kama hii ifuatayo:-

Hussein Wamaywa alizaliwa katika *Hospitali ya Maweni* iliyopo katika *Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Mkoani Kigoma tarehe 27, Julai' 1980.* Alisoma shule ya *Msingi Kiezya mwaka 1991 ha*di 1997, Mwaka 1998 alijiunga na Kituo cha Ujiji Sekondari alikohitimu elimu ya Sekondari mwaka 2001. Baadae mwaka 2004 alisomea Jinsia na Maendeleo katika Chuo cha Mtandao wa Jinsia na kupata cheti kilichomuwezesha kujiunga na Chuo cha Dhahabu Film Art College mwaka 2005 ambako alitunukiwa Stashahada ya Utayarishaji na Utengenezaji wa Filamu mnamo mwaka 2007. Pia amepata kozi fupi fupi za utunzi wa kazi za ubunifu kutoka Idara ya Sanaa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na ana cheti cha Uandishi wa Habari alichokipata kutoka Royal College of Journalism (RCJ). Kwa zaidi ya miaka kumi sasa Wamaywa amekuwa akifanya kazi na magazeti mbalimbali kama Mtunzi, Mshauri, Mwandishi na Mhariri. Huu ukiwa upande mmoja, upande wa pili Wamaywa ni mwanaharakati wa Haki za Binadamu, Jinsia na Maendeleo na Mwezeshaji ngazi ya Jamii na amefanya kazi na Mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi katika kupigania maenedeleo endelevu ya watu walioachwa pembezoni na mfumo wa maisha kazi anayoendelea nayo hadi sasa.

Kwa sasa Wamaywa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mfuko wa Fasihi Tanzania unaolenga kurejesha hadhi ya fasihi nchini na kuifanya fasihi kuwa zana muhimu ya maendeleo ya jamii. Pamoja na mambo mengine, Mfuko wa Fasihi ndiyo pia unaoandaa Tamasha la Fasihi ya Kiswahili ambalo linafanyika mara moja kila mwaka.

*Kususu Tuzo ya Mabati, alikuwa na haya ya kuzungumza.*

Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Kiafrika, (Kwa sasa inaitwa Safal Cornell) ni tuzo inayolenga kutambua kazi bora na nzuri zilizopo katika lugha ya kiafrika. Tuzo hii hutolewa kila mwaka kwa miswada bora, ambayo haijawahi kuchapishwa katika tanzu za riwaya, ushairi, wasifu na riwaya za picha. Miswada inayoshinda huchapishwa na shirika la uchapishaji vitabu la East African Educational Publishers (EAEP). Na mswada bora wa ushairi hufasiriwa kwa

kwa Kiingereza na kuchapishwa kitabu na shirika la Africa Poetry Book Fund. Tuzo hii inadhaminiwa na kampuni ya Mabati Rolling Mills, Kenya, na kampuni ya ALAF Limited, Tanzania (ambazo ni miongoni mwa kampuni za Safal Mauritius Limited); pia na Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Maswala ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Cornell, na Idara ya Taaluma za Afrika ya Chuo Kikuu cha Cornell, Marekani. Nikirudi katika swali lako, waandishi wengine wanatakiwa kuwa na ubunifu wa hali ya juu katika visa vyao na waviandike kwa umahiri ili kuleta mantiki katika maandishi yao. Hata hivyo wanapaswa kutambua yale ni mashindano na katika mashindano wote mnaweza kuwa bora, lakini ni lazima apatikane mshindi. Hivyo kukosa Tuzo haina maana kwamba wewe sio mwandishi mzuri.

*Pia alieleza mazingira mazima ya mwandishi wa riwaya yanavyokuwa kwenye kutayarisha kazi zake. Unaanza nini na kipi kinafuata?*

Labda niseme kwa upande wangu naamini utunzi wa riwaya ni kipaji na kipaji hakina muundo maalum ambao unaweza kusema utaufuatisha kila wakati. Hapa nina maana utayarishaji wa kazi za sanaa na pengine fasihi hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine. Kwangu mimi huwa ninaanza na wazo (idea), wazo hulipata popote katika vitabu vya watu wengine, katika mzungumzo ya kawaida ya kila siku, kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na kwingine kwingi, na wakati mwingine katika tafakuri za kawaida za kila siku. Nikipata wazo huwa naliandikia muhtasari kwa ufupi (Rejea kitabu cha Mkakati wa Kuelekea Ikulu na EPA). Baada ya hapo huanza kukisuka kisa cha awali kabisa (Skeleton) cha mkasa huo.

Baada ya hatua hii, taaswira ya riwaya yangu huanza kuonekana na ni katika hatua hi ndipo ninapofanya utafiti wa masuala yanayohitajika ili kuipa riwaya yangu uhalisia na kuifanya ilete mantiki kwa watakaoisoma. Ninapokamilisha utafti, kazi ya kuandika huanza (hapa tunaanza kuweka nyama katika ile Skeleton yetu). Huwa naandika maneno 500 hadi 1000 kila siku asubuhi na mapema baada ya kuamka. Riwaya ikikamilika hujipa muda na kuisoma kwa mara ya pili huku nikiiboresha zaidi.

Baada ya kuridhika nayo huwa ninaipeleka kwa Mhariri kwa ajili ya uhariri. Ikitoka kwa mhariri, huboreshwa tena (iwapo kuna maboresho) baadae ndiyo taratibu za kuichapisha huanza. Nimesema huu ni muundo wangu binafsi.

*Upande wa idadi ya vitabu alivyovitoa.*

Nadhani vinaweza kuwa saba au vinane hivi. Ndiyo ni vinane ambavyo vimechapishwa, Vitano vya riwaya na vitatu vya kijamii. Katika Riwaya nimeandika zifuatazo; Kauleta Nani? Siku Isiyo na Jina, Mkakati wa Kuelekea Ikulu, Mapenzi Yamelogwa na EPA= Eleza Pesa Alipozificha. Vitabu vya Kijamii ni Ndoto za Lowasa, Kusimama Tena Bila Mume na Wanawake Mashujaa wa Kolelo Morogoro. Aidha ninazo riwaya kadhaa ambazo hazijatoka ambazo ni Moyo wangu Unaungua, Nipe Roho yako, Kivuli cha Huzuni, Wasalimie Kuzimu na Simulizi fupi ya Malkia wa Mikosi.

*Kilichomsuku kuandika kitabu cha MKAKATI WA KWENDA IKULU ni hiki.*

Kuna wakati Wastaafu wa Iliyokuwa Jumuia ya Afrika Mashariki waliandamana na kuvua nguo hadharani wakishiniza Serikali iwalipe mafao yao. Kitendo kile cha kuandamana na kuvua nguo hadharani huku wakipigwa na FFU kilinigusa sana, nikafikiri mtoto wa mstaafu ambaye atakuwa anasoma/ameajiriwa au yuko katika madaraka atakuwa mtu wa namna gani baada ya tukio lile? Ni hapo lilipokuja wazo la kuandika mkasa ule. Mkakati wa Kuelekea Ikulu unazungumzia ufisadi na uzandiki walioanao wanasiasa ambao huimba nyimbo nzuri jukwaani hali maisha yao halisi yakiwa tofauti na kile wanachohubiri. Wengi ni wezi wa mali za umma, mafisadi na watu wenye kiu kali ya utajiri. Mkakati pia unazungumzia namna jamii inavyoshiriki kuwatengeneza mafisadi wa kesho, ni riwaya ya kipepelezi iliyosheheni mapigano na mambo mengi ya Fasihi. Ni riwaya inayowataja kwa majina watu mashuhuri kama Mwalimu Nyerere, Marais Wastaafu Jakaya Kikwete na Benjamin Mkapa. Aidha vyama kama CCM, CUF, Chadema na UPDP vimetajwa kwa namna ya kuvutia sana pamoja na viongozi wao akina Philip Mangula, Freeman Mbowe, Profesa Ibrahim Lipumba n.k

*Zitto Kabwe aliwahi kusifia kitabu chake hadharani. Ni hali gani aliyojisikia baada ya kusifiwa. Alisema haya.*

Nilifurahi sana. Zitto Ruyagwa Kabwe mtu makini na ni

na ni msomaji mzuri wa vitabu, hivyo kusoma kitabu cha mwandishi mdogo asiye na jina kama mimi na bado apate muda wa kukichambua na kukichapisha gazetini ilikuwa zaidi ya faraja kwangu. Ni bahati mbaya ameshindwa kunipa fursa ya kuandika kitabu cha maisha yake.

*Siri ya kutunga majina mazuri ya vitabu kama vile EPA.*

Hiki pia ni kipawa kingine. Jina la riwaya linatakiwa kuvuta hisia, mtu akilisoma tu atake kujua ndani yake kuna nini. Na kwa sisi tunaoandika riwaya za masafa marefu ambazo hazina picha hata moja ndani yake, jina ni muhimu mno. Lakini kwangu mimi huwa naanza kusuka kisa na kupitia maandishi huwa Napata jina. Mara chache nimeruhusu mashabiki zangu wanichagulie majina. Jina kama MAPENZI YAMELOGWA kwa mfano lilichaguliwa na mashabiki wangu kwa ushauri mkubwa kutoka kwa ndugu yangu katika fani Kevin E. Mponda.

*Kutegemea vitabu kama sehemu ya kipato. Alikuwa na haya.*

Kwangu mimi katika Mapato na uuzaji wa kazi za fasihi kuna changamoto kubwa, kuna wizi, na udhulumati. Hakuna daraja zuri kati ya watunzi na wasomaji. Likijengwa daraja zuri baina yetu na kukawa na usimamizi wa kutosha, bila shaka tutakivuka kikwazo hiki. Na kwa kwetu sisi tunayo kampeni ya Kitabu kila mahali, natumai pia kampeni hii inaweza kupindua meza kibabe na tukaanza kunufaika na kazi zetu.

*Waandishi wanayemvuti zaidi.*

Navutiwa na wengi sana. Kwa kizazi kilichopita nilivutiwa sana uandishi wa Ben R. Mtobwa, Elvis Musiba, Eddie Ganzel, Shaaban Robert na Beka Mfaume. Kwa kizazi cha sasa navutiwa na wengi ila uandishi wa George Iron Mosenya, Laura Pettie, Fadhy Mtanga na Japhet Nyang'oro Sudi huwa unanikosha zaidi.

*Na mtindo wake wa utunzi aliweza kuugusia.*

Kwa kweli natumia mitindo ya aina tofauti tofauti kulingana na mkasa ninaouandika kwa wakati huo. Ila ninapenda sana kuandika katika nafsi ya tatu kwa kuwa inakupa wigo mpana wa kuwatazama wahusika wako na kuwaratibu kwa mujibu wa kisa chako katika namna inayomfanya msomaji wako abaki na taharuki kwa muda mrefu.

*Waandishi wawili ambao akiambiwa awachague waandike naye kazi, aliwataja hawa.*

Ningemchagua Beka Mfaume na Hussein Tuwa.

*Tofauti ya uandishi wa riwaya, na uandishi wa simulizi ya filamu. Alizungumza hivi.*

Riwaya ni chakula kilichokamilika, wakati hadithi ya filamu ni chakula kinachosubiri watu wengi zaidi kukikamilisha. Riwaya unaiandika peke yako, lakini hadithi ya filamu utaanza kuiandika hadithi yake, aje mwingine kwa Script ya wahusika (Dialogue), aje mwingine kwa Script ya kupigia picha, mwingine kwa script ya kuhariria n.k. Mwisho wa siku unaweza kuletewa filamu uliyotunga ukaikataa kuwa siyo ya kwako.

*Huu ndio mwisho wa makala hii maalum iliyoandaliwa na Markus Mpangala. Tunawashukuru wote kwa ushirikiano wao.*


TULIZO MEDIA

**TULIZO MEDIA**

***Ni Muunganiko wa Kazi Sita.***

***1. Tulizo Graphics. Kazi yake ni kufanya kazi zote za ubunifu kama vile kufanya majalada ya hadithi, riwaya, tamthiliya, nyimbo, ushairi, kupanga kitabu, kuandaa mipango ya biashara nk.***

***2. Tulizo Studio, hii ni kwa ajili ya kuandaa kazi za sauti.***

***3. Tulizo Magazine. Hili ni jarida linaloruka kila mwezi.***

***4.Tulizo Printing. Kazi yake ni kuchapa kazi mbalimbali.***

***5. Tulizoflix. Huu ni ulimwengu wa filamu ambapo tulizo huzichambua.***

***6Tulizo Visual. Hapa ni kwenye kutengeneza videos na kupiga picha mbalimbali zenye viwango.***

***Kwa huduma wasiliana nasi kwa +255 627 585 638***

MSOMAJI WETU

# NEEMA MBILINYI MGAO NILIANZA DARASA LA KWANZA NA MIAKA 14

Naitwa Neema Elias Mgao, ingawa mitandaoni kama facebook, natumia Neema Mbilinyi Mgao ( Mbilinyi ni jina la ukoo nilikoolewa)


Nina umri wa miaka 37.

Nimeolewa( ndoa ya mke na mume mmoja kwa maana ya ndoa ya kanisani).

Mimi ni mama wa watoto wanne. Wawili wanangu wa kufikia kwa Waswahili wanaita watoto wa kambo, ingawa silipendi hilo jina eti wa kambo ila ila Mswahili aelewe basi tuache hivyo. Na watoto wawili ni wa kuwazaa mimi mwenyewe.

Usomaji wa vitabu nilianza muda mrefu sana. Kwanza nilichelewa sana kuanzishwa shule, nimeanza darasa la kwanza nikiwa na miaka 14. Sasa hapo mahali walezi wangu walikua wamepanga kulikua na familia moja tulitokea kuelewana nayo sana. Baba wa familia akawa ananiona nashika sana magazeti, lakini kwakuwa sijui kusoma nikawa nageuza maandishi, yaani kichwa chini miguu juu. Hivyo akawa akipiga kelele sana na walezi wangu kuwa wanipeleke shule. Wakati huo mlezi naye anasema mtoto wa kike yake ndoa tu. Lakini nashukuru yule jirani alishinda hivyo nikaanzishwa shule nikiwa mkubwa, binti wa miaka 14 nd'o naanza darasa la kwanza. Kilichosaidia ni kuwa nilikua mfupi. Nilipojua kusoma, yule jirani sasa akatoka kwenye kuniletea magazetini mpaka akawa akiniletea majarida ya michoro kipindi kile majarida ya kina baba ubaya yapo kwenye chati, lakini isivyo bahati yule jirani aliuwawa na majambazi. Nikajikuta nimepoteza nguvu ya kusoma, hadi nilipoingia sekondari (Dodoma Sekondari) nikaanza kusoma upya. Na hapo nikaanza na kuandika pia. Mungu aendelee kumpumzisha mahali pema peponi uncle Julius (Baba Jack).

Kuhusu idadi ya vitabu navyosoma kwa mwaka, inategemea na mwaka unavyokuja, unavyoishi, na kuondoka. Mwaka ukiwa hauna rabsha sana naweza






naweza kununua na kusoma vitabu zaidi ya 180. Lakini ikiwa tofauti inaweza shuka kidogo, ila si chini ya vitabu 150. Mfano, mwaka huu nimenunua vitabu 120 kutokana changamoto za hapa na pale nimesoma 112 tu.

Kiuhalisia usomaji wa vitabu nchini unaendelea kupanda siku hadi siku, hii ni kutokana na uhamasishaji kutoka kwa waandishi mbalimbali wa fasihi na mitandao pia inachangia kukuza usomaji. Hivyo sio mbaya sana.

Mbali ya kuwa ni msomaji wa muda mrefu lakini pia Mimi ni mwandishi. Hadi sasa kabatini nimeshaandika vitabu vitatu. Viwili vipo vinaendelea kupikwa, ila kimoja tulishirikiana na mwandishi mkongwe/nguli ndugu yangu Suleiman Kijogoo, kitabu kiliitwa USIGEUKE NYUMA ambapo baadaye kilipofanyiwa marekebisho kikatoka tena kwa jina la JIJENGE KISAIKOLIJIA.


Pamoja na uchache wa wasomaji, haohao wachache walikipokea vizuri sana, hata inaendelea kunishawishi kutoa na kingine na kingine tena. Ila mapokeo yalikua mazuri sana.


Nikisimama nafasi ya msomaji,

nawashauri waandishi kuwa wabunifu na kuzidi kuandika uhalisia maana kuna watu amini usiamini wanaishi kutokana na maandishi wanayosoma.

Bahati nzuri nilishakua na nafasi serikalini, katika ngazi ya serikali ya mtaa. Ilikua kila mwezi walau nimnunulie mtu kitabu kimoja pale naponunua vitabu vyangu, na ni tabia ambayo sijaiacha hadi leo, ingawa kidogo nimetoka kwenye mfumo, lakini kwa kuwa nimewahi kuwa kiongozi, mfumo haujaridhia kuniacha mazima. Bado nimebakia katika baadhi ya mambo. Lakini pia naendelea kuhamasisha usomaji kwa namna moja au nyingine.

Kitabu cha ISHINDE TABIA YA KUGHAIRISHA MAMBO cha mwandishi kaka JOEL NNANAUKA, utafikiri alikua ananisema mimi mle ndani, na nashukuru saana angalau kimenibadilisha kutoka kwenye ukilema, sasa nipo napambana kuendelea kujiponya kwenye tabia hiyo.




Mimi ni mzuri saana wa kuandika usiku, yaani ile mida ya kuanzia saa saba usiku hadi Saa kumi alfajiri aisee hapo akili huwa kwa kiwango kingine kabisa kwenye kuandika, hivyo nikiwa na ratiba ya kuandika huwa naandika mida hiyo.
Kusoma huwa nasoma sana mchana, na sina mahali maalumu, yaani hata kwenye daladala mie kama nasoma nitasoma tu.

Asante.

Madame Neema Mbilinyi Mgao.
Dodoma.
Tanzania.

*Maelezo haya yametokana na sisi kuuliza maswali na yeye kuyajibu. Tunamtakia kila la kheri mwanamama huyu katika safari yake ya uandishi na kusoma.*

TULIZO MEDIA

**TULIZO MEDIA**

***Ni Muunganiko wa Kazi Sita.***

***1. Tulizo Graphics. Kazi yake ni kufanya kazi zote za ubunifu kama vile kufanya majalada ya hadithi, riwaya, tamthiliya, nyimbo, ushairi, kupanga kitabu, kuandaa mipango ya biashara nk.***

***2. Tulizo Studio, hii ni kwa ajili ya kuandaa kazi za sauti.***

***3. Tulizo Magazine. Hili ni jarida linaloruka kila mwezi.***

***4.Tulizo Printing. Kazi yake ni kuchapa kazi mbalimbali.***

***5. Tulizoflix. Huu ni ulimwengu wa filamu ambapo tulizo huzichambua.***

***6Tulizo Visual. Hapa ni kwenye kutengeneza videos na kupiga picha mbalimbali zenye viwango.***

***Kwa huduma wasiliana nasi kwa +255 627 585 638***

# MAKALA MAALUMU

# EROTOMANIA: UGONJWA WA AKILI USIOTAJWA UNAOSUMBUA WENGI




NA GODFREY MAKARANGA

**Katika maisha ya kila siku kuna watu wanapitia mambo mbalimbali ya kimwili na hata yale ya kihisia.**

**Baadhi hupata hisia za kuhisi na kufikiri anapendwa na mtu fulani ilhali kiuhalisia haiko hivyo.**

**Mfano unaweza kukuta mwanamke au mwanaume anaamini anapendwa na mtu fulani maarufu au mwenye uwezo kiuchumi. Imewahi kukukuta au imemkuta mtu wako wa karibu?.**

**Hili ni moja ya tatizo la akili na baadhi ya watafiti zinasema huwa linawaathiri sana wanawake kuliko wanaume. Hawakuweka bayana sababu zinazosababisha kuwa juu kwa wanawake kuliko wanaume. Huku baadhi ya tafiti zikionyesha kuwa Wanaume huwa ndiyo wahanga wa hali hii mara nyingi.**

**Kitaalamu hali hii hujulikana kama EROTOMANIA au Clérambault Syndrome- Hii ni kutokana na Daktari wa magonjwa ya akili aliyejulikana kama Gaëtan Gatin Clérambault.**



***Baadhi ya sababu zinazoweza kuchochea hali hii ni kama;***

**- Kukosa kujiamini.**
**-Upweke na kuhisi kukataliwa.**
**-Kujitenga na jamii.**
**-Mawazo Wakaeleza kwamba yaweza kuwa kichocheo kikubwa cha hali hii.**

***Baadhi ya Dalili zake ni;***

**-Hisia kali za kuhisi unapendwa na mtu fulani hasa wenye hadhi wakati kiuhalisia haiko hivyo.**
**-Kujaribu kutengeneza ukaribu na mtu huyo.**
**-Kuamini kwamba wanawasiliana kwa siri hata kimoyo moyo.**
**-Kumuonea wivu.**
**-Kuwa tayari hata kupigana na kutukana hadhari kwaajili ya mtu huyo.**

**Tatizo hili linatibika kwa dawa na kwa Tiba ya utambuzi wa tabia (Cognitive Behavioural Therapy).**



# Heshima Muhimu

Na Hussein Mwinshehe




Inafikia hatua eti mwandishi anamwogopa msomaji. Kasomaji kanakuja kwenye kazi ya mwandishi kanakashifu, kanatukana, kanadharau kazi ya mwandishi halafu mwandishi mwenyewe unakuta eti anakaita kasomaji hako kaka.

NDUGU YANGU

Mwandishi wewe ni binadamu kama yeye. Una moyo kama yeye. Una akili kama yeye. Umeumbwa kama yeye. Kwa nini ukae unavinyenyekea visomaji? Kwa sababu vinanunua kazi zako? Au sababu vinasoma? Acha hizo bwana, maandishi yako hayahusiani na maisha yako wala mwili wako ndio maana unaandika uchawi lakini we si mchawi. Akikutukana mwondoe kwenye listi ya watu wako.

Tusifanyane kama watoto. Eti kisa kioo cha jamii, basi sitakiwi kurudisha majibu pale napotukanwa. Msomaji asikumiliki mwandishi kisa vijisent. Wewe ni mkubwa kuliko hata huto tujisenti twa kununulia kabeji na chainizi.

Jivunie heshima yako. Sio atokee tu mtu aje na kuanza ooh, hujui kuandika bwege wee. Eti unauza hadithi lenyewe bayaa. Mara nyenyenyeee. Kangafu kabisa.. Pasua mtu akileta ujinga..

Ifikie muda kama hupewi heshima, ichukue heshima yako kwa nguvu. Baadhi ya watu akili zao hazifanyi kazi bila kushtuliwa na viboko. Ukimpa mmoja boko la uso, hawa wengine watakutazama kwa jicho la tatu, aidha waku-unfriend au wajiheshimu au nao wakuvamie. Wakikuvamia piga wote mboko.

Hilo chaguo la kwanza.

La pili ni hili.

Waandishi jengeni mazowea mazuri na wasomaji. Hawa ndio kila kitu kwenu. Inapotokea wanakukashifu, kukutusi au kufanya lolote ambalo halikupendezi, kwanza cool down. Pili fahamu kuwa hao ndivyo wanavyokosoa. Tatu tazama ni wapi hasa umekosea hadi wakunange namna hiyo. Kisha fanyia kazi mapungufu. Endapo wote tungekata tamaa na maneno ya wasomaji, basi fasihi ingelala.. Hakuna mwandishi ambaye hajapitia shuruba za wasomaji wenye masimango na makasiriko yao. Wengine walitusimanga na kutukashifu lakini leo ndio mabesti zetu. Hivyo ndivyo sanaa ilivyo.. Uki complicate masimango ya wasomaji, utadanja kisanaa mapema sana.

Mwandishi unayeanza, jiepushe na skendo hasa za kuiba kazi, kunakili, kuiga, skendo za ngono na zingine ambazo zitakudharaulisha kwenye macho ya jamii. Penda kushirikiana na wengine. Waheshimu waliokutangulia na ambao umewazidi. Unapopata nafasi ya kuwasaidia, wasaidie kwa moyo mmoja.

Usisahau kumwomba MUNGU akuongoze kwenye kila jitihada zako ambazo unazifanya.

FASIHI SIMULIZI

# LEYLAT MBOYA TOKA USEKRETALI HADI UMALKIA WA SAUTI

Muite Leylat Mboya, ama kama unaona shida, mtunuku cheo cha Malkia wa Sauti. Hakika huyu ni Malkia hasa mwenye sauti yake. Kwa wale ambao wamesikiliza baadhi ya hadithi alizosimulia, huwaambii kitu kuhusu sauti mororo aliyoumbwa nayo mwanadada huyu. Lakini unajua historia yake? Ndicho kimetuleta hapa.

Amezaliwa miaka 25 iliyopita, yaani ana miaka ishirini na mitano tu! Ni mtoto wa pekee kwa mama yake na ni mtoto wa kwanza kati ya watoto saba wa baba yake. Yaani mwanadada anadeka kwa mama lakini kwa baba kule, anakutana na wa kudeka wengine.

Elimu yake bwana, ana cheti cha usekretali. Lakini bidada huyu anasema ana historia ndefu ya misukosuko ya maisha na taaluma. Kwa kuwa sisi tupo hapa kifasihi zaidi, tumeona tubaki kwenye nyanja hiyo lakini ipo siku tutamsaka ili atuletee hadithi yake ya maisha hasa ile ya mapenzi.

Basi mwanadada anasema kuwa, safari yake ya fasihi ilianza baada ya kukutana na Abra Tuesday. Yeye mwenyewe anasema bila kificho kuwa Abra ni dereva wa safari yake ya awali ya fasihi. Jamaa alimfanya aingie rasmi katika kazi ya fasihi na kuigeuza sauti yake kuwa pesa. Wewe ndugu msomaji unaye nani aliyewahi kuigeuza sauti au mikono yako iwe pesa? Kama unaye, hongera sana kwako. Ila mwanadada, yeye alionyeshwa njia. Hiyo sauti unayotumia kulalamika huna pesa, mwenzako aliigeuza na kuwa kipato. Umeona mambo hayo?

Leylat anasema, tangu akiwa binti mdogo alipenda kusomea wenzake vitabu. Hii ilikuwa ni huko shuleni, nyumbani na kila mahali. Pia alikuwa na ndoto ya kuwa mhariri mkubwa ndani na nje ya Tanzania. Lakini bahati haikuwa upande wake, ndoto ziliyeyuka baada ya kuhimu elimu ya upili 2014. Hatujui kwa nini ndoto zilititia namna hiyo lakini sisi kama Tulizo, tunaamini ndoto bado zipo na yeyote anaweza kuziamsha na kuzitimiza. Tunamsihi mwanadada, asikate tamaa.

Anaendelea kusema kuwa, moyo wake ulizaa tumaini jipya baada ya kuwa mtunza nyaraka. Mnamo 2017 nikahitimu kozi ya usekretali ngazi ya cheti. Akiwa anasubiri ajira, alijihusisha na vibarua mbalimbali lakini utamu zaidi ni kuwa alipata ajira katika kampuni ya Aitel kama sekretali.

Hapo akapata kuwa katika kundi moja la Whatsapp la Firensa Aitel. Akawa na mchezo wa kuwasomea simulizi na watu wakavutika na hiko kitabia chake. Kwa hiyo ikawa desturi sasa, kila baada ya kurudi kutoka kazini anawasomea simulizi kwa sauti. Raha iliyoje jamani. Unasomewa simulizi bure kabisa

2018 akaingia rasmi katika tasnia baada ya kukutana na Abra Tuesday katika moja ya makundi yake ya whatsapp. Huko wakaanza rasmi kazi ya sauti. Simulizi yake ya kwanza kuitia sauti iliitwa 4G - Mnara wa Raha. Sipati picha ilikuwaje huko kwenye mambo ya 4G na limnara lake la maraha. Bwana wee, hayatuhusu.

.

Baada ya hiyo simulizi sasa, milango ya kazi ikafunguka barabara. Huku na huku, huko na huko mambo hayakwenda vema kabisa baada ya kujaribu kwenye makampuni mengi sana. Lakini siku moja ambayo haina



jina, alikutanishwa na mwanadada mwingine mwenye sauti ya hakshi, takshishi na balaa zito, huyo ni bibie Fety Diva ambaye huyu sasa alikuwa mbele zaidi yake. Alikwishamtangulia katika kazi hii ya fasihi simulizi.

Hapo akapata wasaa wa kuingia SIMULIZI MIX na kuanza kutambulika kama Leylat Mboya. Lakini kutokana na umahiri wa kubadili sauti anaposimulia mashabiki wakaona isiwe tabu, wakamtunuku taji la Malkia wa Sauti. Raha iliyoje? Mtu unasimulia hadi wasikilizaji wananyoosha mikono juu na kukutunuku jina maridadi kama hilo. Hakika mwanadada ana haki ya sauti yake kumlisha.

Anasema tayari kaweka sauti kazi za waandishi mbalimbali. Na kwa sasa ni mwajiriwa wa SIMULIZI CLUB. Baadhi ya kazi alizoweka sauti ni pamoja na:-

-Nikipata Nauli
- Njia Yangu Iliyojaa Mateso
- Why Me
- Chumba cha Siri
- Kurudi kwa Moza
- Nakumbuka Mama
- Hitimisho la Dhuluma
- Hatma Yangu
- Uko Wapi Mama na nyinginezo nyingi.

Tulizo Media tunamtakia kila la kheri Leylat katika kazi zake zingine. Na kwa yeyote anayetaka kufanya kazi za sauti na binti huyu, anakaribishwa sana.



# CHEKA NA TULIZO

## NAOMBENI USHAURI

JUZI muda wa saa nane, nilipata ruhusa toka kazini kwangu ili nirudi nyumbani baada ya kujisikia vibaya. Kwa kawaida huwa natoka kazini saa 11 jioni. Juzi niliwahi kwa sababu ya hiyo hali.

Ninaishi na mpenzi wangu mwaka wa pili sasa. Nampenda sana. Lakini sikumwambia kuwa nawahi kurudi. Na hata wakati nafungua geti dogo ili niingie kwenye uzio wa nyumba yangu, hakusikia lolote.

Nilitembea kivivu hadi kwenye mlango wa kuingilia ndani ambapo kwa hapa mwanzoni huwa ni jikoni, na pia kuna sehemu ya kuoshea vyombo. Nilipotaka kukishika kitasa tayari kwa kukiminya niufungue mlango, nilisikia sauti ya mpenzi wangu ikitokea sebuleni kuja pale jikoni. Alikuwa anawasiliana na mtu kwa njia ya simu. Nilitega sikio kwa makini ili nisikie alichokuwa anakizungumza maana nilisikia akitaja neno Mganga Mpya.

"Shosti naosha vyombo. Ngoja nikuweke laudispika." Mpenzi wangu aliongea na hakusubiri kujibiwa, akaweka hiyo laudispika. Nikasikia sauti ya mwanamke.

Naijua vema hiyo sauti. Ni ya rafiki yake. Tena yule aliyesimamia kidete suala la mimi kumchukua mpenzi wangu niishi naye kabla hata sijatambulika kwao.

"...Nakwambia huyo kiboko Bi Shoshisto. Mmeo hata akinusa harufu ya ushuzi wako, lazima adate. Sembuse akila hicho kimediko kwenye chuzi lililoungwa kwa nazi. Likakolea futa la Korie. Umeweka ndimu na kapilipili kakuwasha mshawasha, nako kanatabahi kwenye rosti la kuku." Sikuwahi kudhani kama huyu dada ana maneno namna ile tena maneno ya Kipwani Pwani.

Licha ya kusikitika kutokana na ushauri wake, ila nilijikuta mate yakinijaa kwa hamu ya hicho chakula alichokuwa anakihadithia.

"Tena anapenda pilau balaa." Mpenzi wangu akapamba yale maongezi. Moyo ukapiga paa. Mi kwa Pilau, unaweza kuniteka kirahisi kinoma.

"Sasa imagine..." Huyo Bi Shosho wake akaendelea. "Hapa pembeni pilau. Pale kachumbari yenye hoho, na ile pilipili ya kunukia. Hapa rosti kuku wa kienyeji lina kidawa cha Mama Kibwende. Anachomoka huyo?"

"Haki ya MUNGU sichomoki." Nilijisemea moyoni.

"Akichomoka huyo, nahama duniani naenda kuishi kwenye Mekyuri." Swali nililojiuliza hapo ni kama yale maneno kayatoa mpenzi wangu ama nani. Nikataka kuchungulia dirishani ili nihakiki, ila nikahisi atadeku uwepo wangu hapo. Huwa haongei kabisa maneno kama haya. Loh!

"Sijamaliza mama..." Rafiki yake akadandia.

Nikatega sikio tena nikasogeza na kichwa changu hadi sikio likagusa mlango ili nipate utamu wa maongezi. "Hapo kabla hajaanza kula sasa, wewe unakuwa umevaa kikhanga chako kimoja halafu unamnawisha kwa mikogho yote. Hakikisha maji yanakuwa ya moto hadi ashindwe kuyanawa..." Nikarudi nyuma kidogo. Nikaona huyu sasa ana nia mbaya na mimi huyu. Hata mpenzi wangu aliliona hilo.

"Hee! Kisa cha kumuunguza ni nini?" Mpenzi wangu, ambaye kwenye simu nimemsevu Pipi na ile namba nyingine nimemsevu Koni. Najua mwenyewe kwa nini nimemsevu hivyo; aliuliza.

"We nawe?" Huyo shosho wake akamshushua. "Unakuwa kama zezeta uzezetani..." Akaendelea. "Hapo unatafuta sababu ya kumwongelesha tu. Akifanya aishiii. Unamuuliza umeungua? Hapo lazima utizamwe usoni..." Moyo wangu ukajikuta unaruka kichura chura. Namjua vema Pipi wangu. Uso wake akiamua kuupara, mchepuko unaweza kumaliza vipodozi vyote duniani lakini usimfikie.

"Sasa na wewe unakuwa umeshapaka wanja wako, kope zimekolea shedo. Midomo umeipaka malipu shine, unawaka kiasi kwamba hata umeme ukikatika nchi nzima, unaweza kuitwa wewe na kuwekwa kwenye gridi ya Taifa." Akachombeza huyo shosho.

"Wee! Mke wangu kwenye gridi ya taifa. Nitateka Ikulu." Nikajiwazia huku naendelea kumsikiliza huyo mwamba wa kike.

"...Jicho lilegeze huku umelitumbua. Sauti itoe kama umebanwa na kabali ya jambazi. Akisema ndio naungua.. Jifanye unaondoka kwenda kuchukua maji ya kupoozea. Hicho kikhanga chepenga kama chandarua na navokujua kwa hizo dunia mbili ulizozibeba peke yako, akichomoka siku hiyo, haki basi yeye ni jini."

"Shosti una visanga wewe." Mpenzi wangu aliongea kwa kwa hali ya furaha huku nje mimi nipo hoi kwa sababu sijui ya ule ugonjwa niliorudishwa nyumbani ama yale maongezi ya hawa marafiki.

"Lazima macho yawe yanatazama hiyo mirindimo utakayokuwa unaimwaga wakati unatembea kwa madaha kama Twiga mwenye donda kwenye kwato. Na wewe unageuka nyuma ili kuhakikisha kama anakutazama. Kama anakuangalia, ng'ata kucha kama kigoli mzoefu."

"Shosti umenishinda tabia. Kha!" Pipi aliongea na mimi nikaungana naye."

"Ukileta maji sasa. Mnawishe kwa bashasha. Baada ya kumaliza mkalie mapajani. Chukua shingo ya kuku ama firigisi, mlishe. Vidole vyako si vitakuwa na mchuzi mchuzi, mlambishe taratibu..." Kiukweli yule shosho ni mwongeaji. Aliongea mengi tu.

"Kwa hiyo lini tunakwenda?" Akauliza My Pipi baada ya porojo nyingi.

"Wewe tu. Hata sasa hivi..." Akajibu Shosho wake.

"Leo hapana. Labda kesho." Moyo ukanilipuka tena.

"Ni kweli mpenzi wangu mshirikina?" Nikajiuliza. "Hapana."

"Kesho saa nne hivi. Nitakupitia hapohapo." Akaongeza rafikiye. "Tena nitamshauri Bibi mwenyewe akupe na khungu. Akupe na mafusho ya kukunukisha mwaka mzima. Yaani wewe, embu ngoja niache." Hadi hapo nikawa nimejua nia ya mpenzi wangu.

Ili asijue kama nimesikia, ikabidi niondoke kabisa pale nyumbani. Nikaenda kwenye kioski kimoja na kuagiza chips kuku pamoja na soda. Nikala.

Nilirudi nyumbani muda wa siku zote. Mpenzi wangu alinipokea kwa bashasha zote kama kawaida. Tukasalimiana lakini chakula nilitaka kula usiku maana muda huo nilikuwa tayari full. Kesho yake ambayo ni jana, nilikwenda kazini ila mawazo bado yakawa yamenitanda. Nilitamani kumshirikisha rafiki yangu wa karibu, ila nikaona kama nitamuaibisha mpenzi wangu.

Sasa leo nilimpigia simu mpenzi wangu na kumwambia kuwa nitawahi kurudi. Na kweli, mida fulani nimerudi hapa home. Nimekutana na picha ileile ambayo shosho wake alikuwa anamwambia. Kakopi na kupesti kila kitu. Na mimi bila kumuangusha aliyeandika skripti, imebidi nitendee haki fani yetu ya kuigiza. Hapa navyokwambia, nimeshakula sahani nusu na kuku nimemaliza wote. Nimekuja huko bafuni kuandika huu ujumbe.

**JE? NIRUDI KUMALIZA ILE PILAU AU NIACHE? NILE VINGINE.**

**NAOMBENI USHAURI.**

# FUKUFUKU



## YUPO WAPI SWEDY SHAURI?

**2015 HADI 2017 kijana huyu alipata umaarufu mkubwa kwa kazi zake mbalimbali za uandishi. Aliweza kuandika riwaya na machombezo mbalimbali kwa muda lakini baadaye akapotea katika tasnia ya uandishi.**

**Mara kwa mara alidai masomo yalikuwa yanambana lakini hata baada ya kumaliza masomo, bado hakuonyesha nia ya kurudi kwenye uandishi na badala yake aligeukia fani ya kutengeza midundo ya muziki (Beats) katika studio zake.**

**Na baada ya hapo, alipotea kabisa na mtandaoni. Hakuonekana kirahisi na hata kwenye kuta zake za mitandao zinaonekana kutoguswa kwa muda sasa.**

**Tulizo Media kupitia Jarida lake la Tulizo, tumemkumbuka sana mwandishi huyu aliyebamba vema na kukonga nyoyo za wasomaji wengi..**

**Hatujui alipo, lakini kama kuna yeyote ambaye anafahamu uwepo wake, tunaomba atutaarifu ili tumpe ujumbe wetu kuwa tasnia ya uandishi bado inamuhitaji.**

# HABARI NAZI




## IPO KESHO WA SALUM MAKAMBA, APAA

**Kupitia ukurasa wa Swahili Stori unaopatikana kwenye Jarida la Twiga ambalo husambazwa na Precision Air, shirika la ndege lililipo Tanzania, karuka kijana toka UWARIDI; Salum Makamba.**

**Hii inakuwa mara nyingine tena kwa mwandishi toka UWARIDI kupata nafasi ya kuruka kwenye ukurasa huo.**

**Hadithi yake fupi inamuhusu kijana masikini kwa jina Ipo Kesho. Kijana huyo ambaye familia yake ilitelekezwa na baba yao, anajikuta peke yake baada ya mama na nduguze kufariki pia.**

**Ipo Kesho anamsaka baba yake lakini kule alipo anakutana na manyanyaso ya kupindukia. Anakimbia na mwishowe anajikuta anakuwa mwandishi nguli Tanzania na dunia nzima.**

**Soma kisa kizima kwenye jarida la Twiga.**

**Za chinichini ni kuwa huyu jamaa anaweza kutoa kitabu chake cha kwanza muda si mrefu. Hiyo nimekumegea tu ili ujiandae.**


## *TULIZO MEDIA*

***Ni Muunganiko wa Kazi Sita.***

***1. Tulizo Graphics. Kazi yake ni kufanya kazi zote za ubunifu kama vile kufanya majalada ya hadithi, riwaya, tamthiliya, nyimbo, ushairi, kupanga kitabu, kuandaa mipango ya biashara nk.***

***2. Tulizo Studio, hii ni kwa ajili ya kuandaa kazi za sauti.***

***3. Tulizo Magazine. Hili ni jarida linaloruka kila mwezi.***


***4.Tulizo Printing. Kazi yake ni kuchapa kazi mbalimbali.***

***5. Tulizoflix. Huu ni ulimwengu wa filamu ambapo tulizo huzichambua.***

***6Tulizo Visual. Hapa ni kwenye kutengeneza videos na kupiga picha mbalimbali zenye viwango.***

***Kwa huduma wasiliana nasi kwa +255 627 585 638***

# 3 ZA KUKUTULIZA




**CHOZI LA MWISHO:** Erick Mbise, mwandishi wa vitabu mbalimbali vya Kiswahili na Kiingereza, anakuja na Chozi la Mwisho ambacho kinaelezea masaibu yaliyomkuta kijana wa kiume hadi kupelekea kumwaga chozi, ambalo yeye kaliita chozi la mwisho.

Kwa kujua kisa hiki kwa undani, basi nunua kitabu hiki ambacho pia kinapatikana kwa lugha ya Kiingereza kwa jina la The Last Tear.


Ni Erick Mbise na Chozi la Mwisho. Wasiliana na uongozi wa Tulizo tukuelekeze pa kukipata kitabu hiki.




**NDEGE TUNDUNI:** Riwaya nyingine toka kwa Mwandishi Japhet Nyang'oro. Ni riwaya ya kijasusi iliyojaa visa na mikasa ya kusisimua.

Mwandishi huyu ambaye amekwishatoa vitabu vingine zaidi ya kumi, anafikisha habari njema kwa wasomaji wake kwa kuwaambia tayari NDEGE TUNDUNI kinapatikana nchi nzima kwa shilingi elfu kumi na tano za Kitanzania (TSHS.15,000)

Kwa taarifa zaidi pa kunyakua nakala zako, wasiliana na uongozi wa Tulizo.




**MONEY BANK:** Rajab Said, ulikwisha msoma hapa kwenye Jarida la Tulizo kwenye upande wa Mjasiriamali na pia umemsoma kwenye safari yake ya kuandika hiki kitabu cha Money Bank.

Ni kitabu kilichosheheni matukio ya kukata na shoka. Matukio ya kusisimsha na yale kukufanya upagawe. Kitabu hiki kinaendelea kupatikana kwa bei ya shilingi elfu kumi na mbili (TSHS. 12,000) na kinapatikana popote pale nchini. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na uongozi wa Tulizo.

# ULIMWENGU WA TULIZO



2019, mwanamama wa Kibrazil; Silvia Grecco, alishinda tuzo ya shabiki bora wa FIFA baada ya kuonekana jukwaani akimwelezea mwenendo mzima wa mechi mwanaye wa miaka 11 ambaye ni kipofu.



Rais wa kwanza wa Zimbabwe alieyeitwa Rais Banana (Ndizi) aliunda sheria ya kuwakataza wananchi wasilitanie jina lake.



Mwaka 2013, jamaa mmoja huko China alitakiwa kulipa kiasi cha Dola 1600 kwa kosa la kutukana. Kwa kiburi jamaa alitoa pesa hizo kwa njia ya sarafu. Iliwachukua waajiriwa 18 kuhesabu pesa hizo siku nzima.




Jamaa mwenye sauti ndogo duniani, Ndugu Tim Storms anaweza kutoa sauti ambayo masikio yetu hayawezi kuisikia.



Huko Singapore, bigijii (Bazoka) huuzwa kwenye Duka la Dawa pekee na kwa kibali maalum toka kwa Daktari.



Huko Finland, mtoto aliyezaliwa anarudi nyumbani akiwa na boksi lililokuwa na vitu sitini (60) zikiwemo nguo, mashuka, mablanketi, midoli, vitabu huku hilo boksi likiwa na uwezo wa kugeuzwa na kuwa kitanda cha kupumzikia



Huko Italia unafungwa mwaka mmoja au kulipa faini ya EURO 10,000 kama utamfukuza/kumtupa paka au mbwa.




Magereza ya Scotland huwanunulia wafungwa wake Playstaions 5 na XBox ili wajiburudishe.

Tulizo Printer. Wanachapa aina zote za dokumenti kuanzia vitabu, nyaraka mbalimbali, wasifu, tawasifu na kila aina ya dokumenti. Bei zao ni rahisi mbapo kila mteja anaweza kuzimudu bila shida. Kwa muhitaji wa huduma, anaweza kuwasiliana moja kwa moja na Tulizo Media kupitia email ya tulizomedia@gmail.com au kwa whatsapp +255 752 353 039. Karibuni.

# Pilipili ya Embe

**Sophia Hamad**

**PILIPILI YA MAJI LITA MOJA**

**Mahitaji**

*1.Pilipili Mbuzi 50*
*2.Vinega ili pilipili isiharibe*
*3.Kitunguu Swaumu kimoja*
*4.Kitunguu Maji kikubwa kimoja*
*5.Tangawizi iliyotwangwa*
*6.Maembe makubwa matatu, yasiwe yameiva sana*
*7.Chumvi kijiko kimoja, Malimao mawili*
*8.Chumvi, Ndimu au Limao*
*9. Mafuta ya kupikia vijiko vitano vikubwa.*

**Hatua za Mapishi:**

*1. Katakata maembe yako na kuyaweka kwenye sufuria safi.*
*2. Kata pilipili pia. Pilipili moja itoe vipande vinne.Weka kwenye sufuria pia.*
*3. Tenga kwenye sufuria lenye maembe na pilipili, kisha mwagia vinega nusu ya kikombe cha chai.*
*4. Pika pilipili yako taratibu huku ukiichanganya kwa tangawizi, vitunguu swaumu na vitunguu maji.*
*5. Hakikisha vimewiva kabisa na kuwa laini. Viepue na kusubiri vipoe ndani ya dakika kumi.*
*6. Vikipoa kiasi, vimwagie kwenye brenda na kuanza kusaga. Hakikisha vimesagika vizuri kabisa kiasi cha mbegu za pilipili kutoonekana.*
*7. Chukua mchanganyiko uliousaga ambao utakuwa ujiuji, mwagia kwenye sufuria lingine safi.*
*8. Weka mafuta yako ya kupikia vijiko vitano kisha acha pilipili ichemke tena safari hii kwa muda mrefu zaidi.*
*9. Epua pilipili yako baada ya kuhakikisha kuwa imechanganyika vema na mafuta ya kupikia.*
*10. Rudisha kwenye brenda safi kisha isage kwa mara ya mwisho huku ukiongeza kidogo vinega.*
*11. Weka pilipili yako kwenye kidumu cha lita moja au kwenye vikopo mbalimbali vya kuhifadhi vimiminika tayari kwa matumizi.*



# DUNIA TAMBARA BOVU


IMELETWA: SAFINA SALIM

MAWASILIANO: +255 623 398 039


"Bibi nisaidie," Ilisikika sauti ya binti mdogo akiwa kitandani. "Mgongo unaniuma bibi, mwili wangu unaniuma, nimechoka naomba nishike mkono ninyanyuke. Bibi leo tena tunaenda kupasua kokoto? Baba na mama wangekuepo nisingeteseka hivi. Bibi, kwanini waliniacha? Natamani kwenda shule bibi kama wenzangu." Binti akiwa amevalia sura ya huzuni iliyoambatana na hasira aliongea huku machozi yakitiririka.

" Bibi mimi leo sitaweza kubeba kokoto mwili unaniuma." Bibi akifuta machozi kwa maneno makali aliyokua akiyasikia kutoka kwa mjukuu wake.

"mjukuu wangu tutakula nini? Mama yako alikuacha." Bibi akimeza mate kwa uchungu. "Ni miaka minne sasa. Hajanitafuta wala hajarudi sijui yuko wapi! Ni mzima au yuko hai sijui, simu yangu ndio ile imekua mbovu kwa hiyo hata mawasiliano hakuna.

Hata mimi nimechoka mjukuu wangu, umri wangu umeenda kazi ya kupasua kokoto ni ngumu sana inaumiza mwili lakini nitafanyaje? Natamani uende shule lakini nani atanisaidia kazi za pale? Lakini nitajitahidi uende shule mjukuu wangu."

Bibi akinyanyuka pale kitandani "ngoja nikoroge uji tunywe tuondoke."

Akamshika mkono. "Maisha yana siri kubwa, na hii dunia ni tambara bovu, haya maneno si sahihi kukueleza kwa umri wako lakini naamini utanielewa tu, sina wa kumueleza." Bibi akiongea kwa uchungu zaidi.

"Lakini sisi hata mlo wa mchana ni changamoto, tunaenda tunaponda kokoto lakini hela ni ndogo. Na ukitaka angalau upate hela ujaze lori, kitu ambacho kwa umri wangu ni ngumu. Unaona mikono yangu ilivyopasuka kazi ngumu pesa ndogo, nataka mjukuu wangu usome. Hizi kazi ni kwa ajili ya watu wazima kama sisi, ambao hata shule hatukuenda au hata kama tulienda, lakini ndo hivyo na ya dunia tukaona kusoma hakuna maana."

"Yaani nikiamka asubuhi," bibi akijinyoosha, "Mwili umechoka ila sasa nitafanyaje? Tutakula nini? Ndio maana nataka ukasome, angalau ukisoma mjukuu wangu ukipata kazi hata ukiumwa mshahara wako unaingia, tofauti na kutokusoma mvua, jua lako."

Wakiwa njiani yule binti mdogo akawa anatembea lakini akilalamika, mara ashike mgongo mara kiuno kwa sababu ya uchovu.

"Nakueleza mambo haya mjukuu wangu kwa sababu sina wa kumueleza wewe ndio mfariji wangu." Bibi akiwa ameshika nyundo.

"Ndugu zangu wote wametangulia mbele za haki." Binti yule akamuuliza bibi yake huku akijinyoosha.

"Kwani kutangulia mbele za haki ndo nini?"

Bibi akamuangalia mjukuu wake akamuambia, "mjukuu wangu kutangulia mbele ya haki ni kuondoka duniani yaani unapotea katika dunia hii. Utayajua haya unavyozidi kukua. Kuna muda na mimi natamani kuondoka, ila natamani niendelee kuwepo kwa ajili yako. Nawaza hatima yako, sitaki uishi maisha haya, usiteseke kama mimi. Umri huo ni wa wewe kuwa shule." Bibi akiwa anakaa chini anaendelea kuponda kokoto.

"Ngoja nifanye mpango niende

shule leo, tufanye kazi kidogo twende hadi shuleni. Endelea kukusanya kokoto hizo hapo."

Binti yule akachukua karai kuukuu lakini wakati anachukua analalamika, "bibi nimechoka lakini." Akakaa chini huku analia.

Bibi akiwa anashusha nyundo yake na kupandisha, jasho jembamba likianza kumtoka. "Leo ikifika saa sita, naona likipita gari moja likichukua hizi nitakazokua nimepasua, tuondoke twende shuleni."

Binti akafurahi sana, akashusha shingo yake kulia kushoto." Bibi ngoja tufanye haraka twende".

Binti akachukua karai harakaharaka akaanza kumsaidia bibi yake.

Bibi akamuangalia mjukuu wake huku anatabasamu. Moyoni akijisemea. "Masikini mjukuu wangu, kumbe kanapenda sana shule, nisingewaza kumpeleka ningekua nimemkatili haki yake ya msingi kabisa."

"Twende shuleni mjukuu wangu, nikaongee na mwalimu mkuu wa shule. Nina amini utaanza kusoma kama wenzako. "Akifuta jasho

"unajua ukisoma mjukuu wangu, kunakua na afadhali na unafuu wa maisha. Tofauti na ukiwa hujasoma, usiposoma nguvu ya mwili itatumika zaidi."
Binti yule alibaki anamshangaa bibi yake!

"Lakini bibi, nitakuacha mwenyewe hapa? Nani atakusaidia?" Binti machozi yakianza kumtiririka. Bibi akamfuata na kumfuta machozi, akiwa amemshika mashavuni.

" Usilie mjukuu wangu, mimi pia nimekuzoea katika kazi yangu hii." Akimsogezea macho yake karibu na macho yake, wakitizamana kwa ukaribu. " Kusoma ni kwa faida yako sitaki uje uteseke kama mimi sitakisitaki."

Bibi akiwa ameinamisha kichwa chini wakati huo, akimkumbatia.

"Wewe ni binti unatakiwa usome sana uwe na chako, uwe na uwezo wa kujihudumia wewe mwenyewe usitegemee kuhudumiwa na mtu. Utasoma utafika mbali mjukuu wangu hii kazi nitaifanya mimi, ili ukirudi shule upate chakula."

Bibi akauza debe mbili za kokoto kwa siku hiyo, wakaondoka wakiwa na mavazi yao yale yale na ndala zao kuu kuu. Wakaelekea shuleni pana umbali mrefu sana, lakini hatimaye walifika. Kwa sababu shule yenyewe kwa majengo haiko vizuri imechakaa sana. Wanafunzi pia wamevaa nguo zilizochoka na ndala chafuchafu. Walimu pekee ndio walionekana katika mavazi nadhifu.

Bibi alienda kwa unyonge sana akawauliza watoto, wakiwa wanamshangaa sana mwenzao. Katika wanafunzi wale kuna mmoja huwa anamuona na jina anamjua akamuita, "Yasmini!"

Mtoto kwa sababu ya furaha ya kufika maeneo yale alimkimbilia kwa bashasha, akaitika "abee! Na mimi nimekuja shule nataka nisome kama nyie."

Bibi akaenda hadi ofisini kwa mwalimu mkuu, akamkaribisha. "Karibu sana bibi."

bibi akajibu "asante sana mwanangu, nimekuja na mjukuu wangu huyu, naomba aanze kusoma ana umri wa miaka nane. Mimi napasua kokoto ndo ninachotegemea sana ananisaidia sana lakini, nimeona nimlete shule. Kupasua kokoto yale ni maisha yangu. Huyu nataka asome, mwalimu naomba nisaidie sina hela ya ada wala hela ya kushona sare ya shule."

Mwalimu kwa muda wote huo alikua anamuangalia bibi, kwa masikitiko sana. "Bibi sasa hivi usijali kwa sababu elimu ni bure, hata hivyo ulikua unamnyima mtoto haki yake ya msingi kabisa. Nakupongeza sana bibi kwa hatua uliyoamua kuchukua. Wengine wapo na watoto wanawatumikisha tu wanaona ni sawa lakini sio sawa kabisa, mtoto kama huyu anatakiwa awepo shuleni. Kwani wazazi wa mtoto wako wapi? Kwa sababu,

"mwalimu akikuna kichwa." nikiangalia umri wako kumfuatilia mtoto ni changamoto, lakini nitakusaidia pamoja na walimu wenzangu, kumfuatilia kwa ukaribu.

"Bibi akivuta pumzi na kushusha." acha tu mwalimu wangu, mama yake huyu ndio mtoto wangu. Aliondoka akasema anaenda kutafuta hela lakini tangu alivyoondoka hajarudi. Ni muda sasa ni mzima au yuko hai sijui, hata mawasiliano hakuna. Ndio maana nikaona nije tu mnisaidie, hata kula yetu ni shida lakini nitajitahidi hivyohivyo na kazi

yangu atakula."

Mwalimu mkuu akamjibu "sawa bibi usijali mtoto lazima asome." Bibi akipiga magoti. "Asante sana mwalimu wangu."

Mwalimu kwa mshangao baada ya kuona bibi anapiga magoti. "Bibi simama hili ni jukumu letu kuhakikisha kwa mazingira yoyote yale, mtoto anasoma."

Bibi akamgeukia mjukuu wake. "mjukuu wangu mwalimu huyu hapa, naomba usome uzingatie masomo, usije ukawa kama mimi."

Mwalimu akiwa anapapasa juu ya meza yake, kuangalia kama kuna kalamu. " njoo mtoto mzuri, unaitwa nani?"

Mtoto akiwa kainamisha kichwa chini. "Naitwa Yasmini". Akishika vidole vyake vya mkono.

Mwalimu akamuuliza "unapenda kusoma?"

Yasmini akajibu. "Napenda sana mwalimu."

Mwalimu akamuambia, "basi sawa, utaenda darasa lile pale, uanze kusoma na wenzako."

Mtoto akakimbia kawafuata wenzake, na ukawa mwanzo wa Yasmini kuanza kusoma.

Mwalimu akamuambia bibi. "Sasa bibi huyu utamuacha hapa, huyu muda mchache uliobaki aanze kuzoeana na wenzake. Nyumbani anapajua?"

Bibi akipandisha kichwa chini juu ishara ya kukubali "anapajua na kuna wenzake ni wa maeneo ya karibu kule atakuja nao."

"Sawa bibi." mwalimu akamjibu.

Miaka ikasonga Yasmin akasoma akamaliza akapata na kazi. Lakini wakati amepata kazi, bibi tayari alikua ameshafariki. Yasmini akiongea huku analia, macho yake yakiwa mekundu sana.

"Natamani bibi yangu ungekuwepo ila haupo, umeniacha nimepata kazi lakini hujafaidi matunda yangu. Nilitamani ungekuwepo, uvae utakavyo, Mungu naomba mrehemu bibi angu. Nimeamini dunia tambara bovu, unazaa mtoto unalea kwa taabu zote, anapata kazi halafu Mungu anakuchukua mapema.

Na hii ndio dunia kila mtu ataondoka kwa wakati wake. Pumzika kwa amani bibi."

MWISHO.

# MTEGO WA KIFO

## MTUNZI: NELSON NTIMBA

ANGALIZO: RIWAYA HII INAPATIKANA YOTE
KWA BEI NAFUU. WASILIANA NA MWANDISHI
MAWASILIANO: +255 656 353 765

---

*ILIPOISHIA.*

*Baro aliguna. “Usinipe ushauri.” Alisema, “Ninafahamu kipi naweza kufanya na kipi siwezi.” Baro akasimama. “Naona niondoke. Na usisahau ikitokea kuna jambo lolote la kuingiza hela nistue. Kwaheri.” “Mbona umekuwa na haraka ghafla?” Henry alisema.*

*“Ninataka niondoke kabla Mjomba Sama hajaamka. Sina hela ya kumnunulia chakula akistuka na kunikuta nipo humu.”*

ENDELEA.

Baro alienda hadi ilipo meza ya mapokezi na kumlipa Yule msicha hela ya alichotumia na kutoka nje ya mgahawa. Jua lilimpokea na kumpiga kama ngumi. Ukilinganisha na ile Whisky aliyokunywa alihisi kizunguzungu. Aliingia ndani ya gari na kuwasha sigara, huku akili yake ikiwa bado inakimbia.

Ikitokea, neno likavuja kuhusu huo mkufu, kila kibaka wa mtaani atatamani afanye jambo. Je, Frank angekuwa na ubavu wa kuifanya hiyo kazi.

Alimstua Mjomba Sam. “Oya!” Aliropoka. “Una tatizo gani wewe? Sikuhizi kazi yako ni kulala muda wote tu.”

Mjomba Sam, mwenye umbo refu, na akitafuta umri wa miaka sitini, aliyafumbua na kufumba macho yake mara kadhaa kabla hajaamka na kuketi vyema.

"Tunaenda kula, sio?"

"Nimekwishakula." Baro alijibu.

"Na mimi je?"

"Nenda kale kama una mkwanja. Mimi sikulipii." Baro alilalamika. Mjomba sama alishusha pumzi ndefu. Akakaza mkanda wake wa abiria na kuisogeza kofia yake.

"Kuna tatizo gani sasa hivi, Baro?" Mjomba Sama alihoji. "Inakuwaje tunakosa kabisa pesa. Nakumbuka zamani tulikuwa tunapiga pesa. Sasa hivi hatupati kitu kabisa. Unajua naona shida ni nini? Frank anatumia muda mwingi kwa yule malaya wake baadala ya kuweka akili yake kwenye biashara."

Baro aliegesha gari nje ya duka la dawa. "Upumzishe mdomo wako," Baro alisema na kushuka kutoka kwenye gari. Akaingia kwenye kibanda cha simu. Alibofya namba fulani na kuzipigia, na baada ya kusubiria kwa muda kidogo, Frank alipokea simu upande wa pili.

Baro alikuwa anasikia sauti za mziki zikitokea upande wa pili na Anna akiwa anaimba kwa sauti ya juu sana. Hata hivyo, Baro alianza kumwelezea Frank yale aliyoambiwa na Henry. Lakini alikata tama.

"Unasema hauwezi kunisikia?" Alianza kufoka. "Kwanini usizime huo mziki kwanza.?"

Frank alisema, "subiria kidogo." Na kuzima mziki.

Anna alianza kupiga kelele za kulalamika – Halafu muda kidogo, Baro akasikia sauti la kofi na ukimya. Baro akatikisa kichwa chake. Ilikuwa ni kawaida ya Frank na Anna kugombana kila siku.

Frank alirudi tena kwenye laini.

"Sikiliza, Frank," Baro alisema. "Ninakaangika kwenye hiki kibanda cha simu. Hebu acha masihara nisikilize. Ni muhimu sana!"

Frank alianza kulalamika kuhusu joto pia.

"Ninafahamu pana joto," Baro alisema. "Tumepata nafasi ya kuweza kuiba mkufu wenye thamani ya zaidi ya milioni sabini na tano. Binti wa Mariki atakuwa ameuvaa usiku wa leo. Wataenda kulala Golden Slipper yeye na mpenzi wake – wao wawili tu. Nimezipata hizi taarifa kutoka kwa Henry. Unasemaje?"

"Umesema ni kiasi gani?"

"Milioni sabini na tano. Mariki ni milionea. Unasemaje?"

Frank ni kama alizinduka. "Sasa bado uko huko unafanya nini? Rudi!" Alisema kwa furaha. "Tunahitaji kulijadili hili suala. Rudi fasta."

"Nipo njiani nakuja." Baro alijibu na kukata simu. Alipotoka nje ya kibanda cha simu aliwasha sigara yake na alikuwa anatetemeka kwa furaha. Kumbe Frank hakuwa muoga kama alivokuwa anamfikiria. Karibuni wangeanza kushika hela.

Alitembea kwa mwendo wa haraka kurudi alipoegesha gari. Mjomba Sam alikuwa anamuangalia kwa macho ya usingizi.

"Amka, we mzee." Baro alisema. "Karibu mambo yanaenda kuiva."

****

Baro alikuwa anatembeatembea nje ya lango kuu la kuingia ndani ya Golden Slipper. Alifurahia kwamba mwanga wa eneo lile ulikuwa ni hafifu. Ingawa Anna alikuwa ameifua ile suti na shati yake, lakini Baro alijua alionekana kama kituko na alikuwa na wasiwasi kuna mtu atamshtukia na kumfukuza nje.

Hoteli yenyewe ilikuwa imefurikwa na watu kibao. Wahudumu walikuwa bize kumhudumia huyu na yule. Hata viongozi wa wa hoteli yenyewe walikuwa bize na mambo yao kiasi ilikuwa ngumu kumshtukia. Alijisogeza na kujibana kwenye kona mojawapo ambako alikuwa na uwezo wa kuona kila kilichokuwa kinaendelea.

Muda wote alikuwa anaiangalia saa yake ya mkononi. Zilikuwa zimebakia dakika kumi ifike saa sita kamili. Aliendelea kupepesa macho yake kwenye kile chumba. Kwenye lango kuu sasa hivi palikuwa pamezibwa na wapiga picha wane au watatu wakichukua picha za tukio huku wakimsubiria binti Mariki. Yeye mwenyewe hakuwa anamfahamu kwa sura hata kama ingetokea amekutana naye au kukutana na picha yake.

Frank ndiye aliyempangia jukumu la yeye kuingia ndani huku wao wakibakia nje na Mjomba Sam. Mara nyingi alikuwa anawekwa sehemu za hatari kuliko yeyote. Hata hivyo, alikuwa na mpango. Watakapogawana pesa basi ataachana na hiko kikundi! Alikuwa amechoshwa na Frank na Anna. Kwa pesa atakazozipata kutoka kwenye mgao wa mkufu huo, ataanzisha biashara ya

ya kufuga kuku. Kwanza alikuwa amezaliwa kwenye familia ya wakulima na wafugaji na kama isingelikuwa matatizo yaliyomsababisha akafungwa jela miaka mitatu basi asingewahi kukutana mahala popote na Frank.

Ghafla mawazo yake yalikatishwa na sauti ya watu wakiimba wimbo maarufu wa 'heri ya siku ya kuzaliwa.'

Anakuja, Baro alijisemea na kusimamia vidole ili aweze kuona mbele ya umati ule uliokuwa umefurika. Kila mtu alikuwa ametoa macho kwenye mlango wa kuingilia ndani. Wale wapiga picha walikuwa wanasukumana kila mmoja akijaribu kupata engo nzuri ya picha.

Halafu mwanga ukaongezeka na kumuonesha binti Mariki akiingia akiwa kaongozana na mwanamume mmoja mrefu aliyekuwa amevalia suti.

Baro alimuona binti Mariki mara moja tu, moyo wake ukakiri hajawahi kuona mwanamke mzuri kama huyo kabla. Alikuwa na kila kitu ambacho wanawake warembo wanacho na kidogo zaidi.

Uzuri wa binti Mariki ulikuwa umemchanganya kiasi kwamba alisahau kuhusu mkufu tena, lakini kwa pozi alilokaa binti Mariki lilimkumbusha Baro kuhusu mkufu wenyewe.

Shingo iliyokuwa imetameta kwa mng'ao wa almas alizovalia binti Mariki ilimpatia kijasho chembamba usoni. Kwa kuziangalia akagundua umuhimu na thamani yake pindi mkufu ule utakapokuwa umeibiwa. Hili lingekuwa ni dili lao kubwa kuliko. Kila askari mjini atawatafuta wao. Labda asingemshawishi Frank waje kujaribu kuuiba, alijiwazia, huku skijifuta kijasho kilichokuwa kinamtiririka.

Halafu akayarejesha macho yake ilipokuwa meza ya binti Mariki. Alimuona yule mpenzi wake akiwa anakunywa pombe kwa fujo, alikuwa anaenda kuongeza nyingine, kabla binti Mariki hajamshika bega kumzuia, Halafu yule mwanamume akaigida bia yake na kusimama huku kamshika binti Mariki mkono na wakatoka nje ya ukumbi. Jamaa keshaanza kulewa, Baro alijiwaziwa. Halafua akamuona binti Mariki akijitoa kwenye mikono ya Baron a kurudi kukaa mezani. Yule mwanamume akarudi na kukaa mezani pia na kuendelea kunywa bia.

Kwenye meza jirani kulikuwa na mzee mmoja amekaa na binti mmoja wanabishana. Yule mzee alionekana amelewa sana. Yule binti akasimaa juu, akanyanyua bia ya pombe na kummwagia yule mzee usoni. Yule binti akamaliza akaiweka chupa mezani na kukaa chini.

Yule mwanamume akasimama huku uso wake ukiwa unabalika rangi kuwa nyekundu. Wanaume waliokuwa karibu hapo wakaangua vicheko. Yule mzee akabeba bakuli kla chakula lililokuwa mezani pale na kummwagia yule binti – Pembeni akainuka kijana wa makamo tu na kumpiga ngumi yule mzee. Kwa hasira wakazua ugomvi pale.

Walevi! Bags alijiambia. Akayahamisha macho yake Akayahamisha macho yake kumtazama binti Mariki. Binti Mariki alikuwa amesimama anatetemeka huku bwana wake akiwa kamshikilia mkono. Walianza kutembea kutoka ukumbini mule. Alipohakikisha wamelivuka lango la kutokea Baro aliwafuata kwa nyuma na kuwapita na kuelekea moja kwa moja hadi yalipo maegesho ya magari. Mjomba Sam alikuwa ameukalia usukani na Frank akiwa pembeni yake.

"Watatoka nje muda sio mrefu," Baro alisema huku akipanda kwenye kiti cha nyuma. "Nadhani binti Mariki ndiyo atakuwa anaendesha maana bwana wake anaonekana amelewa kupita kawaida."

"Kanyaga mafuta," Frank alimwambia Mjomba Sam. "Tutaegesha kwenye kile kishamba kidogo tulichokipita kipoindi tunakuja huku."


Mjomba Sam alizipanga gia na ile Packard ndogo ikateleza kuondoka. Baro aliwasha sigara na kutoa bunduki yake na kuikalisha kwenye siti ya gari pembeni yake.

"Mkufu anao?" Frank aliuliza.

"Ndiyo."

Frank alikuwa ni mrefu na mwembamba ukilinganisha na Baro. Alikuwa mdogo kuliko wote kwenye kundi, ila mwenye akili inayofikiria kwa kasi sana.

ITAENDELEA TOLEO LIJALO



# TULIZO SPESHO

## MREMBØ NA MNYAMA 2

### IMELETWA; CHRISTINE BELLINGTON

“Ni nani amekuruhusu uchume maua yangu, haikutosha kwamba nimekuhifadhi katika kasri langu hivi ndivyo unavyoonesha shukrani?

Hutaondoka bila kupata adhabu.” Mnyama alisema kwa ghadhabu

“Nihurumie bwana mwenye huruma.
Nilidhani kama bwana aliyenipa chakula na hifadhi wakati wa uhitaji wangu asingechukia iwapo ningechukua ua moja kwa ajili ya binti yangu nisamehe sana.” Mfanyabiashara akamsihi

Mnyama aliposikia neno ‘binti’ alishtuka kwa kujua kuwa ana mabinti. Aliamua kumpa sharti moja zito yule Mfanyabiashara ili kuepukana na adhabu. Alimwagiza alete moja kati ya mabinti zake aishi nae pale kwenye kasri ili awe huru na adhabu.

Mnyama alimpa muda wa mwezi mmoja tu kutekeleza hilo na alimpa yule mfanyabiashara moja ya farasi wake wenye kasi zaidi. Lakini pia alimuasa kuwa huyo binti ni lazima aje kwa kupenda asilazimishwe la sivyo hatampokea kwenye kasri lake na iwapo Mfanyabiashara hatatimiza ahadi yake basi atamfata hukohuko nyumbani kwake.

Pamoja na kwamba alikubali sharti lile ili kuokoa maisha yake lakini hakufikiria kama yoyote kati ya mabinti zake angekubali. Mfanyabiashara yule masikini alianza kurudi nyumbani, farasi alikimbia upesi na kufika kwake muda mfupi tu.

Mabinti zake walimkimbilia na kumpokea. Wale wawili waliulizia zawadi zao kwa shauku isipokua mrembo alimjulia hali kwanza baba yake.

Mara baba akatoa uwaridi kwenye koti lake na kumpatia mrembo. Kisha aliwaeleza mabinti zake kuhusu meli na yote yaliyomsibu kwenye safari yake na namna lile uwaridi lilivyomgharimu.

Binti zake wale wawili walianza kumshutumu mrembo kwa nini alimwomba baba amletee ua!!! Pengine angeomba zawadi nyingine yenye maana hayo yote yasingemkuta baba yao.

Mrembo alianza kulia kwa kujua amesababisha balaa akasema,” Basi nitakwenda na baba ili nikatimize ahadi yake.”

Alikubali kubeba mzigo wote na alikua jasiri na maamuzi yake, alimtia moyo baba yake.
Walipanda farasi na safari ilianza kwenda kwa mnyama.

Wakiwa njiani usiku uliingia. Kwa mshangao mkubwa msitu wote uliangazwa kama vile ulimwengu mzima ulikua ukimpokea.

Punde walifika katika barabara ya miti ya michungwa na kuona kasri ikiwa imetiwa nakshi na taa za kuvutia.

Walipofikia bwalo kuu walikuta moto wa kupasha joto ukiwaka na meza ikiwa imepambwa na vyakula vitamu. Walikua na njaa mno baada ya safari ndefu wote walianza kula, punde wakasikia hatua za mnyama yule akija.

“Habari za jioni Mrembo? ”, Mnyama aliuliza.

“Habari za jioni Mrembo? ”, Mnyama aliuliza.

“Nzuri Bwana Mfalme”, Mrembo alijibu.

“Je umekuja kwa mapenzi yako na utabaki hapa baada ya baba yako kuondoka?” Mnyama alihoji tena.

Mrembo aliitikia ndio, baba yake aliambiwa afuate farasi wake nje na kupewa zawadi ya farasi mwingine aliyepakiwa masanduku ya dhahabu kisha akaenda zake.

Mrembo alifungua mlango wa kwanza kuingia katika chumba kilichopambwa vizuri, alijilaza na kwa muda mfupi tu usingizi ukampata.

Alipoamka asubuhi alikuta meza yake ya kujipamba ikiwa na kila kitu ambacho angekihitaji. Bwaloni alikuta chakula chake, akala.

Baada ya mlo aliketi katika sofa kujipumzisha. Aliwaza namna ambavyo atawekwa kifungoni na mnyama yule milele. Alifikiria zaidi namna gani atajiweka huru baadaye alipitiwa na usingizi.

Ilikua jioni mara akamsikia mnyama akija.

“Habari za jioni Mrembo”, Mnyama aliuliza.

“Nzuri”, Mrembo alijibu.

“Je, unanipenda Mrembo na utakubali nikuoe ?”, Mnyama aliuliza tena.

“Looh!”, Mrembo alishangaa.

“Sema ndio au hapana bila hofu”, Mnyama alisisitiza.

“Hapana”, Mrembo akajibu.

“Sawa kwa sababu hutaki usiku mwema Mrembo”, Mnyama aliaga akaenda kulala.

ITAENDELEA.

## *Special Invitation*

Baajun and The Band  Poetry session on 09th Dec 2022. You are welcomed as our honorable and special guest.
Mr/Mrs/Miss/Prof/Dr/Sir/Madame

FRANK MASAI

.............................................................................

To the Poetry,Music,Art exhibition session that will be held on December at
VIVI FOODS, MBEZI BEACH AFRICANA NEAR BUS STAND.

Friday | 18:00 PM
09 Dec | 23:00 PM

CALL
+255 (0) 684 956 676
baajunpoet255@gmail.com


KAISAL ALLY
20 KALI ZA
NINJA
KWA NAKALA LAINI
TSHS. 3,500
20 KALI ZA NINJA
KAISAL ALLY
SEE FOR ME
MEMORY
BECKETT
CONFESSION
+255 657 772 272
WASILIANA NA SISI SASA
WAHI HARAKA